

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI



**TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA KWA WAHITIMU WA FANI ZA UHANDISI,
UFUNDI SANIFU, MAAFISA WA MAENDELEO YA JAMII NA
MAAFISA HESABU WASAIDIZI**

1. UTANGULIZI

- 1.1 Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency - RUWASA*) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019. RUWASA ina jukumu la kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama kwa kusanifu, kujenga miundombinu ya maji na kusimamia utoaji wa huduma. RUWASA inatekeleza majukumu yake kupitia Ofisi Kuu iliyopo Jijini Dodoma na Ofisi katika ngazi ya Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara isipokuwa Mkoa wa Dar Es Salaam.
- 1.2 Kwa kutambua jukumu la taasisi za Serikali katika kuwajengea uwezo, ujuzi na uzoefu wahitimu wa fani mbalimbali kutoka katika vyuo mbalimbali nchini, na katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi, RUWASA inatoa fursa ya nafasi za kujitolea kwa wanafunzi waliohitimu na kufaulu Shahada na Stashahada ya Ufundi (*Technicians*) katika fani ya Uhandisi wa Maji na Ujenzi na waliohitimu na kufaulu Shahada ya Maendeleo ya Jamii na Stashahada ya Uhasibu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- 1.3 Nafasi zilizopo ni za kujitolea kwa muda wa miezi sita (6) kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Mkoa wa Dar Es Salaam. Baada ya miezi (6), RUWASA inaweza kuongeza muda kutegemeana na mahitaji ya wakati huo, rekodi nzuri ya utendaji kazi na mwenendo wa Mhusika wakati wa kipindi cha awali cha miezi sita (6).
- 1.4 Wahitimu watakaokubaliwa kujitolea watafanya kazi katika maeneo ya **usanifu, ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji.**

2. UWASILISHAJI WA MAOMBI

- 2.1 Mwombaji anatakiwa kuandika kwa mkono barua ya maombi na kutuma kwa Anuani iliyotajwa hapo chini ikiwa imeambatishwa na:-

- (i) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa,
 - (ii) Vivuli vya vyeti vya kuhitimu elimu ya Sekondari na Vyuo vya Mafunzo au Taaluma,
 - (iii) Barua ya Serikali ya Kijiji/Mtaa anapoishi,
 - (iv) Picha mbili (*passport size*) na Maelezo ya Wasifu Binafsi (*Curriculum Vitae*).
- 2.2 Kwenye Wasifu Binafsi, Mwombaji anatakiwa kutaja majina ya Wadhamini 3, anuani na namba zao za simu, ambapo Mdamini mmoja lazima awe ni kutoka Chuo alichosoma.
- 2.3 Katika barua ya maombi, Mwombaji anatakiwa kubainisha chaguo lake kuhusu mkoa anaopenda kwenda kufanya kazi ya kujitolea akianza na **chaguo la kwanza, la pili na la tatu**. Pia, Mwombaji anatakiwa kubainisha chaguo lake kuhusu eneo analopenda kufanya kazi kama ilivyoelezwa kwenye **Kipengele Na. 1.4** cha Tangazo hili. ***Hata hivyo, uamuzi wa mwisho kuhusu mkoa na wilaya ambayo Mwombaji atakwenda na eneo la kufanya kazi kwa maana ya usanifu, ujenzi na uendeshaji, utafanywa na Uongozi wa RUWASA.***

3. MASHARTI YA KUZINGATIWA NA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi ya kujitolea ni lazima awe na sifa za msingi zifuatazo:-

- (i) Awe raia wa Tanzania.
- (ii) Awe amehitimu masomo katika Chuo kinachotambulika na Serikali.
- (iii) Awe amemaliza mafunzo yake ndani ya muda usiozidi miaka 3 tangu alipohitimu masomo yake.
- (iv) Kwa Wahitimu wa Uhandisi, wawe wanatambulika na kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*Engineers Registration Board – ERB*) angalau kuanzia ngazi ya Mhandisi Mhitimu (*Graduate Engineer*).
- (v) Aeleze kwenye barua ya maombi utayari wake wa kufanya kazi katika maeneo ya vijiji.
- (vi) Awe na umri usiozidi miaka 35.

MAOMBI YATUMWE KWA:

Mkurugenzi Mkuu,
Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini,
Jengo la NBC, Tawi la Mazengo, Barabara ya Kuu,
Ghorofa ya Kwanza.
S. L. P 412,
DODOMA.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya RUWASA www.ruwasa.go.tz na Mbao za matangazo zilizopo Ofisi za Mameneja wa RUWASA wa Mikoa na Wilaya, Ofisi za Katibu Tawala Mikoa na Ofisi za Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri zote Tanzania Bara.

Maombi yatumwe kwa njia ya posta au kwa mkono kwenye Ofisi Kuu za RUWASA na Ofisi za Mameneja wa RUWASA wa Mikoa na Wilaya Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **26 Machi 2021** saa **9:30 Alasiri**. ***Waombaji wanaokidhi sifa na kuzingatia masharti yaliyotajwa hapo juu ndiyo watakaofikiriwa.***

Limetolewa na:



Eng. Clement KIVEGALO
MKURUGENZI MKUU